



Haydom Lutheran Hospital

ELCT Mbulu Diocese

23/01/2024

TANGAZO LA ZABUNI YA KANTINI

Mkurugenzi mtendaji Hospitali ya kilutheri Haydom anapenda kuwatangazia wazabuni wote wenye sifa na uwezo kutoka ndani na nje ya Mkoa wa Manyara kwamba anakaribisha maombi ya mzabuni kwaajili ya kutoa huduma ya chakula katika kantini iliyopo ndani ya eneo la Hospitali kwa ajili ya watumishi, wagonjwa na ndugu zao na wateja wengine wote watakaohitaji huduma hiyo kuomba zabuni hii..

Hospitali ya Kilutheri Haydom ipo katika kata ya Haydom, Halmashauri ya Mbulu vijijini, mkoa wa Manyara. Hospitali ipo kilomita 50, kutoka makao makuu ya Halmashauri na kilomita 150 Kutoka makao makuu ya mkoa wa Manyara (Babati). Hospitali ina wastani wa watumishi 600 na Jumla ya wagnjwa wapatao 350 kwa siku.

SIFA ZA MWOMBAJI

1. Awe na kampuni iliyosajiliwa
2. Awe na lesini ya biashara (Iliyo hai)
3. Awe na namba ya mlipa kodi (TIN) na aonyeshe eneo lake la biashara (physical address)
4. Tax clearance
5. Cheti cha mamlaka ya chakula, dawa na vifaa tiba (TMDA)
6. Aonyeshe uzoefu wa utoaji huduma ya chakula hasa katika taasisi
7. Awe na wataalamu wenye weledi na kutoa huduma ya chakula (Atoe vyeti vya wataalamu wa mapishi/menejimenti ya hoteli)
8. Cheti cha usajili wa biashara

VIGEZO

1. Awe na uwezo wa kutii au kufuata maadili ya Kanisa la Kiinjili Kilutheri Tanzania





2. Awe na uwezo wa kufuata utaratibu, tunu za Hospitali ya Kilutheri Haydom
3. Mwombaji aambatanishe katika maombi yake tamko la kutojihusisha na vitendo vya rushwa au ushawishi wa aina yoyote ile.
4. Uwezo wa kulipa gharama za kodi kwa miezi sita
5. Uwezo wa kutoa chakula kwa ubora, utoshelevu unaotakiwa wakati wote
6. Kuzingatia usafi wa mazingira ya ndani na nje ya jengo pamoja mavazi yanayokubalika kwa wahudumu
7. Awe tayari kushirikiana na Hospitali katika maboresho ya kantini
8. Awe na mtaji na aonyeshe uwezo wa kifedha kwa tutoa taarifa zake za kibenki
9. Awe tayari kuanza huduma tarehe 01 Machi 2024

Mwisho wa kupokea zabuni ni tarehe 13.02.2024 saa 4:00 Asubuhi. Zabuni zitakazofika baada ya muda huo hazitapokelewa. Zabuni zitafunguliwa siku hiyo hiyo saa tano kamili asubuhi na waombaji wanakaribishwa kushuhudia ufunguzi.

Maombi yote yatumwe kwa:

**Mwenyekiti wa kamati ya zabuni,
Hospitali ya kilutheri Haydom,
S L P 9000,
Haydom-Mbulu
Manyara**

Haydom Lutheran Hospital
P.O. Box 9000 - Mbulu
TANZANIA

**IMETOLEWA NA UTAWALA
HOSPITALI YA KILUTHERI HAYDOM**